

Kifaduro

Kifaduro ni ugonjwa wa kawaida kwa watoto wadogo ambao unaweza kusababisha kupungua kwa njia za juu za hewa kwenye koo. Kelele ya juu iliyotengenezwa wakati mtoto anapumua (inayojulikana kama stridor), na viwango tofauti vya ugumu wa kupumua vinaweza kutokea.

Je, ni nini husababisha kifaduro?

Kifaduro kawaida hutokea katika miezi ya baridi na kwa kawaida hufuata maambukizi ya virusi ambayo huanza na pua yenye kamasi, kikohozi au homa. Kifaduro hutokea wakati maambukizi husababisha uvimbe kuzunguka kamba za sauti (sanduku la sauti) na trachea (njia ya hewa).

Kifaduro ni ya kawaida kwa watoto wa miezi 3 hadi miaka 5 kwa sababu watoto wachanga na watoto wadogo wana njia ndogo sana za hewa.

Nini kinaweza kutokea?

Mtoto wako anaweza kuendeleza dalili za kikohozi kali, sauti ya makohozi na labda sauti ya mapafu (kupumua kwa kelele). Mtoto wako pia anaweza kupata homa. Dalili hizi mara nyingi hujitokeza jioni au wakati wa usiku, na zinaweza kuwa mbaya zaidi ikiwa mtoto wako amekasirika.

Dalili nyingine zinazoashiria hali hiyo zinakuwa mbaya zaidi pamoja na kufyonza ngozi (juu ya mfupa wa matiti, mbele ya shingo na katikati ya mbavu), kukatika kwa pua, na kutokuwa na utulivu. Kikohozi cha kubweka kinaweza kudumu siku chache, na kupumua kwa kelele kunaweza kudumu siku moja hadi mbili.

Nini cha kufanya - utunzaji nyumbani

Wagonjwa wengi wenye kifaduro wanaweza kutunzwa nyumbani.

Ikiwa mtoto wako ana kikohozi cha kubweka tu na ametulia, anafurahi na hajafadhika (kwa mfano anacheza, kula na kunywa kama anavyofanya kawaida), matibabu ya nyumbani yanaweza kujumuisha:

- uchunguzi wa karibu
- kukaa ndani ya chumba cha joto
- msaada na uhakikisho
- dawa za kupunguza maumivu zinaweza kusaidia (kwa mfano paracetamol au ibuprofen - fuata maagizo kwenye chupa).



Virusi vinavyosababisha kifaduro vinaweza kuenea kwa wengine, kwa hivyo weka mtoto kutengwa wakati akiwa mgonjwa, na kudumisha usafi mzuri.

Wakati wa kutafuta matibabu

Ikiwa mtoto wako ana dalili yoyote ya yafuatayo unapaswa kumpeleka kwa daktari wake wa mtaa au idara ya dharura ya karibu kwa tathmini ya matibabu:

- Ugumu wa kupumua (haraka au polepole kuliko kawaida, kufyonza ngozi - kama ilivyoelezwa hapo juu).
- Ugumu wa kula (chini ya nusu ya kiasi chake cha kawaida).
- Anakuwa rangi ya mweupe au rangi ya bluu au ulegevu.

Kifaduro kinawezakana kuwa hatari sana kwani kinaweza kuwa mbaya zaidi haraka. Ikiwa mtoto wako ana dalili zozte za hapo juu, tafuta matibabu ya haraka (unaweza kuhitaji kupiga simu 000 kwa ambulensi).

Matibabu

Kwa kuwa kifaduro husababishwa na virusi, dawa ya antibiotiki haitasaidia. Dozi ndogo za dawa za steroid (dexamethasone au prednisolone) hupunguza uvimbe kwenye njia ya hewa ya mtoto wako kumsaidia kupumua kwa urahisi. Unafuu kutoekana na dalili mbaya za kupumua unaweza kuonekana ndani ya saa moja baada ya kumpa dawa hii.

Mtoto wako bado anaweza kuwa na dalili za ugonjwa wa virusi kwa siku chache baada ya matibabu na dawa ya steroid.

Kesi kali za kifaduro zinaweza kuhitaji dawa za ziada na kulazwa hospitalini.

Je, itatokea tena?

Kifaduro kinawezakana kurudia tena kama kuna baridi inayoendelea. Kila kipindi kinapaswa kuchukuliwa kwa uangalifu kama cha kwanza.

Njia ya hewa ya mtoto wako itakuwa kubwa kadri anapokua na kwa hivyo, matukio ya kifaduro kawaida yatatokea mara chache zaidi baada ya kufikia umri wa miaka 6.

Ikiwa una wasiwasi wowote mwingine mpeleke mtoto wako kwa daktari wako wa mtaa au idara ya dharura.



Government of **Western Australia**
Child and Adolescent Health Service



Huduma ya Afya ya Watoto na Vijana

15 Hospital Avenue, Nedlands, WA, 6009.

Simu: (08) 6456 2222

Imetolewa na: Idara ya Dharura

Kumb: 316.9 © CAHS 2023

Waraka huu unaweza kupatikana katika muundo
mbadala kwa ombi la mtu mwenye ulemavu.

Kanusho: Chapisho hili ni kwa madhumuni ya elimu ya jumla na habari. Wasiliana na mtaalamu wa afya aliyehitimu kwa ushauri wowote wa matibabu unaohitajika.

© Jimbo la Australia Magharibi, Huduma ya Afya ya Watoto na Vijana